Nambari ya Mtahiniwa ____________________

**SMZ**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**MTIHANI WA DARASA LA NNE**

**121** **KISWAHILI**

**MUDA: SAA 2.00** **JUMANNE 26 OKTOBA, 2021 MCHANA**

## MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. **Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.**
2. **Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Swali MOJA (1) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.**
3. **Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
4. **Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
5. **Majibu YOTE yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
6. **Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| **NAMBARI YA SWALI** | **ALAMA** | **SAINI** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

**Mtihani huu una kurasa 11 zenye maandishi**



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A: (Alama 20)

## UFAHAMU

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

1. **Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.**

Hapo zamani wanyama walikuwa wakishiriki katika michezo mbalimbali mara moja kwa mwaka. Wakati huu wa michezo, kila mnyama, ndege na hata samaki walikuwa wanaalikwa. Mfalme Ndovu ndiye aliyepewa **dhamana** ya kutoa kadi za mwaliko.

Baadhi ya wanyama walishiriki katika mashindano ya mbio, kuogelea, kupigana ngumi na mateke na michezo mingine mingi.

Pundamilia kila mara alikuwa akishiriki katika mchezo wa kupigana ngumi na mateke. Mbuni naye alikuwa akishindana mbio zote. Papa alikuwa muogeleaji hodari sana hivyo wanyama wengi **waligonga mwamba** kuivunja rekodi yake katika kuogelea.

Kila mwaka mheshimiwa Kinyonga alikuwa akialikwa kuja kushabikia mchezo wake wa kupigana ngumi na mateke. Mchezo huu aliupenda **mno**. Katika mchezo huu, Kinyonga alipata maarifa mengi, hasa siku ile ambapo Pundamilia alimshinda Simba kwa kumpiga teke lililomuumiza vibaya. Siku hiyo michezo ilifika **kikomo** saa kumi na moja. Washindi wakatangazwa na katibu bwana Ngiri na kutunzwa zawadi **kochokocho**.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## Maswali

a) Wanyama walikuwa wakifanya michezo mara ngapi kwa mwaka?

______________________________________________

______________________________________________

b) Mfalme Ndovu alipewa dhamana gani kwa wanyama wenzake?

______________________________________________

______________________________________________

c) Taja wanyama wawili (2) walioupenda mchezo wa kupigana ngumi na mateke.

i. ____________________ ii. ____________________

d) Kwa nini wanyama wengi waligonga mwamba kuivunja rekodi ya Papa katika kuogelea?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

e) Kinyonga alipata faida gani katika kushabikia mchezo wa kupigana ngumi na mateke?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Jaza maana za maneno yafuatayo kwa kuchagua jawabu sahihi katika mabano.

a) Dhamana ______________________________
(zawadi, jukumu, sifa)

b) Waligonga mwamba ______________________________
(walitaka, waliweza, walishindwa)

c) Mno ______________________________
(kidogo, sana, kiasi)

d) Kikomo ______________________________
(mwisho, karibu, wakati)

e) Kochokocho ______________________________
(nzuri, nyingi, mchanganyiko)

## SEHEMU B: (Alama 40)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

**Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.**

3. Badilisha sentensi zifuatazo kwenda katika wakati uliopita.

i. Juma atakwenda kondeni.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

ii. Sisi tunaotesha mimea.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

iii. Mama atarudi jioni.

______________________________________________

______________________________________________

iv. Kassim anafanya mazoezi.

______________________________________________

______________________________________________

v. Vitabu vitawekwa kwenye kabati.

______________________________________________

______________________________________________

4. Tunga sentensi zenye aina zifuatazo za maneno, kisha pigia mstari aina ya neno lililotumika.

Nambari moja (i) imetumika kama mfano.

i. Kitenzi kikuu

Mama <u>anakuna</u> nazi.

ii. Kitenzi kisaidizi

______________________________________________

______________________________________________

iii. Kiwakilishi cha kuuliza

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

iv. Kivumishi cha sifa

______________________________________________

______________________________________________

v. Kiwakilishi cha idadi

______________________________________________

______________________________________________

vi. Kielezi cha mahali

______________________________________________

______________________________________________

5. a) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Elfu moja mia moja na hamsini na moja.

______________________________________________

ii. Elfu sabini na saba mia saba na sabini na saba.

______________________________________________

iii. Laki mbili elfu sitini na tano na mia tatu.

______________________________________________

b) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

i. I am very tired.

______________________________________________

ii. I don't want to play football.

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

6. a) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

   i. 7,939

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ii. 11,446

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   iii. 24,805

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   b) Taja vyombo viwili (2) vya mawasiliano.

   i. ______________________________________________

   ii. ______________________________________________

## SEHEMU C: (Alama 20)

## FASIHI

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.**

7. Tunga beti nne (4) za ngonjera inayohusu Malezi Bora.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

8. a) Lete maana ya misemo ifuatayo.

   i. Kaa mkao wa kula

   ____________________________________________

   ____________________________________________

   ii. Tega sikio

   ____________________________________________

   ____________________________________________

   iii. Kumtia mkononi

   ____________________________________________

   ____________________________________________

b) Tunga kitendawili kimoja (1) kwa kila jibu ulilopewa.

   i. Kiberiti

   ____________________________________________

   ____________________________________________

   ii. Nanasi

   ____________________________________________

   ____________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D: (Alama 20)

## UTUNGAJI

**Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.**

9. Andika barua ya simu kwa dada yako anayeitwa Hamida Majaaliwa, umueleze kuwa unahitaji pesa kwa ajili ya matumizi ya skuli. Anwani yake ni S.L.P 077, Mbeya.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

10. Jaza vipengele vya barua rasmi kwa kuchagua majibu yaliyomo katika boksi hapo chini. Kipengele nambari sita (vi) kimetumika kama mfano.

| |
|---|
| SAINI, MWANZO WA BARUA, ANWANI YA MPELEKEWA, |
| BARUA YENYEWE, CHEO CHA MWANDISHI, TAREHE, |
| JINA LA MWANDISHI, ANWANI YA MWANDISHI, |
| KICHWA CHA BARUA |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**Nambari ya Mtahiniwa** ____________________

i.

ii.

iii.

iv.

v.

vi. BARUA YENYEWE

vii.

viii.

ix.

===================



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org